

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKIOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA KIGOMA/UJIJI

Simu Na. 028 2802535
Nukushi Na. 028 2802535
Unapojibu tafadhali taja:



OFISI YA MKURUGENZI WA MANISPAA
S. L. P 44,
KIGOMA

**MUHTASARI WA KIKAO CHA MENEJIMENTI (CMT) KILICHOKETI KATIKA OFISI
YA MKURUGENZI WA MANISPAA YA KIGOMA/UJIJI, TAREHE 30/10/2021**

WALIOHUDHURIA

1. Ndugu Fredinand S. Filimbi - Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa -
Mwenyekiti
2. Ndugu Tumsifu G. Kiwoli - Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala wa
Manispaa
3. Ndugu Dismas M. Mgao - Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara wa
Manispaa
4. Dr. John S. Tlatlaa - Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi wa
Manispaa
5. Ndugu Evans Y. Mdee - Kaimu Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji
na Ushirika wa Manispaa
6. Ndugu Issa M. Bukuku - Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi wa
Manispaa
7. Ndugu Shani S. Shabani - Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa
Ndani wa Manispaa.
8. Ndugu Rose A. Choma - Kaimu Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira
wa Manispaa
9. Ndugu Melleji S. Mollel - Afisa Malalamiko
10. Dr. Hashim Mvogogo - Mganga Mkuu wa Manispaa

MUHT. NA. 01/30/10/2021:

KUFUNGUA KIKAO

Akifungua kikao mwenyekiti aliwashukuru wajumbe wote kwa mahudhurio yao mazuri katika kikao hicho. Kikao kilifunguliwa saa nne na dakika kumi (4:10), Asubuhi.

MUHT. NA. 02/30/10/2021:

KUTHIBITISHA AJENDA

Ajenda zilizokuwa zimeandaliwa jumla zilikuwa nne (04) ambazo zilisomwa na kuwasilishwa katika kikao na kisha kuthibitishwa na wajumbe kama ifuatavyo:-

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha Ajenda
3. Taarifa ya mapokezi ya fedha za COVID – 19 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa shule za Sekondari.
4. Kufunga kikao

MUHT. NA. 03/30/10/2021:

**TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA ZA COVID –
19 KWA AJILI YA UJENZI WA MADARASA SHULE
ZA SEKONDARI**

Mkuu wa Idara ya Elimu wa Manispaa (Shule za Sekondari) kwa niaba ya Mkurugenzi wa Manispaa alieleza kuwa, Halmashauri ya Manispaa Kigoma/Ujiji ilipokea fedha za COVID – 19 kiasi cha Tsh. 960,000,000/= (Milioni Mia Tisa Sitini) kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya shule za Sekondari.

Mgawanyo wa matumizi ya fedha kwa jumla ya madarasa 48 (Arobaini na nane) na kiasi kilichotengwa kilikuwa kama ifuatavyo:-

NA	SHULE	MADARASA YALIYOJENGWA	KIASI CHA FEDHA KILICHOPOKELEWA
1	RUBUGA	2	40,000,000.00
2	MASANGA	2	40,000,000.00
3	KIGOMA UJIJI	3	60,000,000.00
4	KASINGIRIMA	3	60,000,000.00
5	KASIMBU	1	20,000,000.00
6	RUSIMBI	1	20,000,000.00
7	MWANANCHI	3	60,000,000.00

8	KATUBUKA		40,000,000.00
9	KIRUGU	2	20,000,000.00
10	KICHANGACHUI	1	40,000,000.00
11	KITONGONI	2	60,000,000.00
12	BUSHABANI	3	80,000,000.00
13	BURONGE	4	60,000,000.00
14	GUNGU	3	80,000,000.00
15	BUZEBAZEBA	4	100,000,000.00
16	BUHANDA	5	80,000,000.00
17	BUHANDA	4	20,000,000.00
18	KITWE	1	80,000,000.00
	BUTEKO	4	960,000,000.00
	JUMLA	48	

Taarifa hiyo iliyowasilishwa katika kikao ilipokelewa na wajumbe na kujadili.

AZIMIO

Fedha kiasi cha Tsh. 960,000,000/= (Milioni Mia Tisa na Sitini) kwa ajili ya ujenzi wa jumla ya madarasa 48 (Arobaini na nane) zillpitishwa kama ilivyoonyeshwa katika mchanganuo ili zitumike kwa mujibu wa maelekezo na kwa kuzingatia thamani ya fedha na kazi (Value for Money) kwa kutumia (Force Account).

MUHT. NA. 03/30/10/2021: KUFUNGA KIKAO

Akifunga kikao mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango yao ya mawazo kuwezesha kikao kumalizika salama.

Kikao kilifungwa saa sita na dakika arobaini na tano (6:45), mchana.

UMETHIBITISHWA

[Handwritten Signature]

MWENYEKITI

[Handwritten Signature]

KATIBU

TAREHE

30/10/2021